
HakiElimu
Waraka wa Msimamo
2011

# Watoto wetu waendelee na masomo baada ya kujifungua:

## Watanufaika wenyewe, watoto wao na jamii




Novemba 2011

hakielimu

# Watoto wetu waendelee na masomo baada ya kujifungua

## Watanufaika wenyewe, watoto wao na jamii nzima

hakielimu

Novemba 2011

## 1.0 Shukrani

Kazi hii ya kitafiti imeandaliwa na kuandikwa na **Mtemi Gervas Zombwe** kwa kushirikiana na **Annastazia Rugaba** wote ni wafanyakazi wa HakiElimu. Hawa walisoma nyaraka, ripoti za kitafiti na vitabu mbalimbali vinavyojadili haki na fursa ya elimu kwa wasichana na mafanikio ya wasichana waliokatisha masomo wanaporejea darasani baada ya kujifungua. Aidha, walifanya mahojiano na wasichana waliokatisha masomo, wahadhiri wa ualimu wa vyuo vikuu, walimu, wanaharakati wa elimu, wazazi na wanafunzi walio shuleni. Tunawashukuru sana wote waliohusika katika zoezi hili.

Shukrani za pekee ziwaendee Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Forest Hill iliyoko Morogoro Manispaa kwa ushiriki wao wa kina kutoa maoni na uzoefu kuhusu suala la elimu ya mtoto wa kike. Hatuwezi kuusahau mchango wa Mkuu wa shule ya Sekondari ya Forest Hill na timu yake ya walimu waliokuwa nasi bega kwa bega hadi kukamilisha zoezi la kufanya mahojiano na wanafunzi. Tunaamini mjadala utakaoendelea kutokana na kitabu hiki  ni matokeo ya mchango wao makini. Tunawashukru sana kwa utayari wao wa kufanyakazi nasi.

Kwa namna ya kipekee kabisa tunatambua pia mchango mkubwa wa akina mama, walezi na wanamaendeleo kutoka Kikundi cha “Tuwe Pamoja Wanawake Kihonda” (TUPAWAKI), kilichopo eneo la Kihonda Morogoro kwa kutoa uzoefu wao, maoni yao na njia halisi za kushughulikia tatizo la wasichana kukatisha masomo. Mama Mariam Magullo, Rehema Ramadhan, Stamili Hussein, Jamila Suma, Basila Kimoto, Zubeda Marcus, Asha Hussein na wenzao ni mifano ya kuigwa kwa wanawake wengi hapa nchini. Wakiwa wanawake, wazazi, walezi pia wasichana wa zamani walitupatia uzoefu mkubwa katika suala la mimba za utotoni na manufaa ya kusomesha mtoto wa kike. Jitihada zao kutetea elimu kwa watoto wetu na maoni yao mazuri waliyotupatia yatawafikia watanzania wengi kupitia chapisho hili.

Mchango wa uhariri umetolewa na Elizabeth Missokia, Elisante Kitulo, Daniel Luhamo wafanyakazi wa HakiElimu.

© HakiElimu, 2011

ISBN: 978-9987-18-025-7

HakiElimu
SLP 79401
Dar es salaam, Tanzania
Simu: (255 22)2151852/3, Faksi: (255 22)2152449

Sehemu yoyote katika kitabu hiki inaweza kutolewa kwa namna nyingine yeyote kwa madhumuni ya kielimu na yasiyo ya kibiashara, kwa kuzingatia kuwa chanzo kitatajwa na nakala mbili ziwasilishwe HakiElimu.

## Yaliyomo

1.0 Shukrani ---------- 2
2.0 Utangulizi ---------- 4
3.0 Hitaji la elimu kwa wavulana na wasichana ---------- 7
4.0 Vikwazo vya elimu kwa wasichana/sababu za kupata mimba ---------- 7
5.0 Kwanini wanafukuzwa shule ---------- 9
6.0 Wakifukuzwa shule wanakwenda wapi na watoto wao? ---------- 11
7.0 Tumefaidikaje na wasichana kufukuzwa shule ---------- 12
8.0 Hasara za kuwafukuza shule ---------- 12
9.0 Kuwarejesha shule baada ya kujifungua: Tunaongozwa na ushahidi au mitazamo? ---------- 15
10.0 Kwanini ni muhimu warudi shule/faida za kuwarejesha shule baada ya kujifungua ---------- 16
11.0 Wanarudi vipi shuleni baada ya kujifungua ---------- 20
12.0 Mbinu za kupunguza mimba kwa wasichana wadogo wa shuleni ---------- 21
13.0 Wapo waliorudi darasani na wakafanikiwa ---------- 24
14.0 Hitimisho na Mapendekezo ---------- 26
*Marejeo* ---------- *28*

## 2.0 Utangulizi

Elimu ni haki ya kwanza kabisa yenye umuhimu mkubwa kwa binadamu yeyote. Kila msichana na mvulana, mwanamke na mwanaume ana haki ya kupata na kunufaika na elimu, na haki ya kufikia matarajio na malengo ya maisha yake. Ana haki ya kujiletea maendeleo yake wenyewe, kujenga maisha yenye ustawi na furaha. Elimu bora ndiyo ufunguo wa yote haya. Elimu inafungua fursa za ajira za kujiajiri na kuajiriwa, ubunifu na fikra za kuthamini na kufanya kazi kwa manufaa ili kuzalisha kipato cha mtu mmoja mmoja, familia na cha taifa. Elimu humwezesha mtu kupanga maisha ya familia anayoitaka yenye afya na ustawi, humwezesha mtu kushiriki kikamilifu katika shughuli za kijamiii, kuinua uchumi wake na kushiriki kikamilifu kwenye amali za taifa na masuala ya utamaduni.

Ni kupitia elimu bora ndipo mtoto wa masikini anaweza kuitawala dunia inayomzunguka! Ni kupitia elimu ndipo mtoto wa kibarua wa mashambani anaweza kuwa Rais[1] wa Taifa kubwa! Ni kupitia elimu ndipo mtoto wa mkulima anaweza kuwa mfanyabiashara mkubwa wa mazao ya chakula duniani! Ni kupitia elimu ndipo yatima anaweza kuondokana na unyanyaswaji na vitendo vya udhalimu! Ni kupitia elimu ndipo binadamu anaweza kutafiti na kuvumbua maarifa na teknolojia mpya.

Kwa manufaa haya, elimu inabaki kuwa kitovu cha maendeleo ya binadamu popote alipo. Na zaidi sana, kwa watu masikini kama zilivyo nchi nyingi za Afrika, elimu pekee ndiyo ukombozi wetu. Hili alilisisitiza sana Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere enzi za uhai wake ambapo alitetea utoaji elimu kwa usawa ili imkomboe mtanzania na anufaike nayo, kama alivyowahi kusema kwamba:

> "....*Kwa watu maskini kama sisi, elimu inapaswa kuwa chombo cha ukombozi..... Ukitaka kumsaidia masikini somesha watoto wake*" (Nyerere 1922-1999)

Tanzania kwa kutambua ukweli huu serikali, wazazi na wadau mbalimbali wa elimu wamewekeza fedha nyingi, jitihada kubwa na muda mwingi kwenye kuhakikisha watoto wetu wanapata elimu. Kwa mujibu wa takwimu za bajeti karibu asilimia 17-20[2] ya fedha zote kwenye bajeti ya taifa zinatengwa kwa ajili ya elimu. Bado kuna asasi na mashirika yasiyo ya kiserikali yamewekeza fedha nyingi kwenye elimu kuchangia jitihada za kuwaelimisha watoto wetu ili wanufaike na elimu hiyo.

Jitihada za wazazi, serikali, mashirika na taasisi mbali zimeshindwa kuzaa matunda tarajiwa hasa kutokana na kuwepo kwa vikwazo vingi vinavyowazuia watoto wetu kunufaika na elimu kwa usawa na haki. Moja ya changamoto kubwa ni kwamba; watoto wetu wengi hasa wasichana, hushindwa kuhitimu ngazi mbali mbali za masomo yao na hivyo kukatisha masomo na kurudi kwenye jamii kuendeleza duara la umaskini.

Nchini Tanzania, kila mwaka zaidi ya wasichana 8,000[3] huacha shule kutokana na mimba. Na maelfu wengine wanaripotiwa kuwa ni watoro kumbe-hawako shule kwa sababu wakipata mimba hawarudi shule kwa kuhofia kufukuzwa. Data za hivi karibuni zinaonesha kwamba idadi ya wanafunzi kuacha shule kutokana na mimba imeongezeka 2008-2009 (MoEVT 2008 & BEST 2010). Na takwimu za Wizara ya Elimu mwaka 2010 zinaonesha shule za sekondari wanafunzi waliokatisha masomo ni

[1] Usemi huu umesisitizwa sana na Rais wa kwanza wa Afrika Kusini Nelson Mandela enzi za utawala wake na harakati za kuikomboa Afrika Kusini

[2] Hotuba za Bajeti 2009, 2010 na 2011

[3] Takwimu za Umoja wa Mataifa Tanzania Julai 2010

66,069[4], japo wengi wao wanaripotiwa kuwa ni watoro, ni wazi kwamba mimba za utotoni ndiyo sababu kuu za utoro huo[5]. Shule ya msingi walikatisha masomo kwa sababu ya utoro(baadhi ni watoro kwa sababu ya mimba) walikuwa wanafunzi 76, 246 na waliofukuzwa kwa sababu ya mimba ni 1,056 (BEST 2011 uk 31).

Taarifa zaidi zinaonesha kuwa hali ni mbaya zaidi kwenye wilaya na maeneo ya vijijini ambako wasichana wengi zaidi huacha shule kuliko maeneo ya mijini. Taarifa kiwilaya zikikusanywa na kunyambuliwa vizuri zinaweza kubainisha hali ya kutisha kuhusu ukubwa wa tatizo hili, lakini kwa bahati mbaya hili halifanyiki kikamilifu. Mathalani, taarifa kutoka Tanga zilionesha kuwa katika mkoa huo tatizo la wasichana kukatisha masomo ni kubwa zaidi. Karibu wasichana 300 walikatisha masomo yao mwaka 2009 kutokana na mimba za utotoni (*Nipashe*: Machi 15, 2010). Mkoani Kagera hali ni ileile, taarifa zinaonesha kuwa wasichana 880 walikatisha masomo yao kutokana na kupata mimba wakiwa shule. (*Jambo Leo:* Januari 12, 2010). Katika mkoa wa Pwani pekee karibu wasichana 500 walikatisha masomo yao kati ya mwaka 2005-2009 kutokana na kupata mimba za utotoni (Jambo Leo, Machi 2010).

Taarifa za Utafiti kuhusu mimba za utotoni kwa wasichana uliofanywa mwaka 2010 na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (TAMWA), zinatoa picha ya kutisha. Mfano, mkoani Tabora pekee Wasichana wa shule 819 walipata mimba kipindi cha mwaka 2006-2009. Na huko Morogoro kati ya mwaka 2007-2009 wasichana wa shule 331 walipata mimba na kukatisha masomo yao[6]. Bado takwimu toka Kitabu cha Takwimu za Elimu Tanzania (BEST 2005-2009) zinaonesha kuwa watoto wa kike walioacha shule kuanzia mwaka 2005-2009 kwa sababu ya mimba za utotoni walikuwa 16,991. Na katika shule za sekondari wasichana walioacha shule kutokana na mimba kwa mwaka 2009 tu walikuwa 4965[7].

Licha ya upana wa tatizo lenyewe kuwa dhahiri kwa kila mtu, kuanzia serikali, wazazi, asasi za kiraia na hata taasisi za kitaifa na kimataifa hakuna taarifa zenye takwimu za idadi ya wasichana waliorudi shule na kuendelea na masomo yao. Takwimu tulizo nazo ni za tatizo lenyewe sio za ufumbuzi wa tatizo[8]. Wote tunafanya kazi kubwa ya kukusanya takwimu za tatizo badala ya kukusanya suluhu ya tatizo ili kulimaliza tatizo lenyewe. Licha ya uwepo wa takwimu nyingi za kutisha na kusikitisha kama nchi, jamii, wazazi na wanaharakati hatujanufaika na takwimu hizo za maelfu ya watoto wetu kukatisha masomo kwa sababu ya mimba. Tumeendelea kuwatumbukiza mabinti zetu kwenye dimbwi la umaskini, ujinga, maradhi na fedheha. Kila mtu anagharimia ujinga wa watoto wetu wa kike wanaokatisha masomo kutokana na mimba za utotoni.

Hatuna ushahidi wa manufaa tuliyopata kutokana na malumbano kuwa warudi shule au wasirudi. Malumbano miongoni mwetu hayajatusaidia kusonga mbele. Maana tunalumbana bila kutafuta suluhu wakati huo watoto wetu wanaendelea kupata mimba wakiwa bado watoto, wanafukuzwa shule, kukatisha masomo na kubaki wajinga wasio na fursa. Muda wa malumbano umekwisha. Karne ya 21 siyo ya malumbano ni ya utafiti, uvumbuzi, na ubunifu kwenye kutafuta suluhu za changamoto! Sasa ni muda wa kutafuta suluhu za kivitendo ili kuwasaidia watoto wetu kuendelea na masomo na kunufaika na elimu.

---

4 BEST 2011 uk 79

5 TEN/MET 2011

Utafiti wa TAMWA kuhusu mimba za Mapema kwa wasichana wa shule, uliofanyika mwezi Aprili 2010 katika mikoa 17 ya Tanzania, umetoa picha ya kutisha kuhusu ukubwa wa tatizo la mimba za utotoni.

7 Takwimu za BEST 2005-2009; Ukurasa 19 & 64

8 Hakuna nchi iliyoendelea kwa kukusanya idadi ya matatizo tu bila kutafuta suluhu na tiba ya matatizo hayo

Bila shaka huu ndio mwelekeo pia wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kama ilivyobainishwa na mwongozo wake wa hivi karibu unaoeleza wazi kuwa kuna idadi kubwa ya wasichana wanaoacha shule, na hivyo serikali ya Tanzania imedhamiria kuruhusu wasichana wenye mimba kurudi shule na kuendelea na masomo yao baada ya kujifungua (MoEVT, Machi 2010). Hatutakuwa wa kwanza kutekeleza zoezi la kuwarudisha wasichana wenye mimba shuleni. Nchi nyingi zinafanya hivyo na faida zimeonekana wazi. Hakuna faida ambazo nchi yetu imepata tangu ianze kuwaondoa shuleni mabinti wenye mimba. Nchi ya Kenya, Zambia na Rwanda ni mifano mizuri ya mataifa yaliyofanikiwa kuwarejesha wasichana wenye mimba shule na wakaendelea na elimu yao kisha wakanufaika nayo. Jambo muhimu ni kuandaa mazingira rafiki yatakayowafanya watoto wetu warejee mashuleni kwa utaratibu mzuri na watoto wao wabaki wakilelewa katika mazingira ya mwendelezo mzuri wa makuzi.

Chapisho hili linaibua hamasa na fikra mpya kwa wazazi, wasichana wenyewe, watunga sera, serikali na wapenda elimu wote kuamua sasa kuwarejesha shule wasichana wadogo wanaopata mimba. Tunawasihi wasomaji kuungana nasi ili kufanikisha adhma hii njema ya kuwaendeleza watoto wetu hasa wasichana kufikia usawa wa kijinsia, kudumisha haki na utu na kujenga nguvu kazi ya taifa iliyo imara itakayoiendeleza nchi yetu.

**Elizabeth Missokia**
**Mkurugenzi Mtendaji, HakiElimu**
**Dar es Salaam, Novemba 2011**

## 3.0 Hitaji la elimu kwa wavulana na wasichana

Dira ya Maendeleo ya Tanzania 2025 inabainisha wazi kuwa "...ili kufikia maendeleo ya kweli Tanzania inafanya jitihada ya kuwa taifa lenye watu wenye shauku na mitazamo ya maendeleo pamoja na ari ya kushindana. Sifa hizi zinajengwa na elimu inayokuza maarifa; na ni muhimu sana kuliwezesha Taifa kuyatumia maarifa katika kuhamasisha kutumia rasilimali za ndani ili kuwa na uhakika wa kuwapatia watu mahitaji yao ya msingi, na kwa kufanikisha ushindani wa kiuchumi kikanda au kidunia. Tanzania itajitahidi kufanikisha ubunifu bidhaa-uvumbuzi na viwango vya juu vya ubora wa elimu ili iweze kuitikia changamoto za kimaendeleo na kuwa na uwezo wa kushindana kikanda au kidunia." (*Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025)*

Elimu ni haki ya msingi ya kila binadamu, kwa sasa ndiyo haki ya kwanza inaweka njia rahisi ya kufikia haki nyingine. Kukosa elimu ni kukosa haki nyingine nyingi. Mathalani, mtu asiyejua kusoma na kuandika anakosa haki ya kupata taarifa na kutoa taarifa kwa njia ya maandishi, anakosa haki ya kuajiriwa, anakosa haki ya kushiriki vyema kwenye masuala ya kijamii, anakosa haki ya uhuru wa maoni na anakosa haki ya kupata maarifa yaliyo kwenye vitabu na maandishi anuai. Wasichana na wavulana wanahitaji zaidi haki hii ili waweze kuutumia kikamilifu uwezo wao. Wizara ya Elimu imebainisha wazi hili kama ninavyonukuu.

"…..Tanzania inahitaji kuwa na wanawake na wanaume walioelimika kikamilifu na wenye uwezo kushiriki kikamilifu kwenye michakato ya kuiendeleza nchi. Kama taifa haliwezi kukaa kando kutoshughulikia suala la wasichana kuacha shule kwa sababu ya mimba, maana linapoteza nguvu kazi muhimu ya vijana inayotoa mchango mkubwa kwenye maendeleo ya nchi"( Mwongozo wa kitaifa wa namna ya kuwawezesha wasichana wa shule kuendelea na masomo baada ya kujifungua, MoEVT, March 2010). Hakuna shaka kuwa katika dunia ya leo kila tasnia ya kiuchumi inahitaji elimu. Mkulima mzuri ni yule aliyesoma, mfanyabiashara mzuri ni yule aliyesoma, mama mzuri ni yule aliyesoma, na mzalishaji mzuri ni yule aliyesoma. Ni elimu tu; bila elimu ni kudhoofisha utu wetu.

## 4.0 Vikwazo vya elimu kwa wasichana/sababu za kupata mimba

**4.1 Hali duni ya uchumi wa familia**. Ufukara na hali ngumu ya kiuchumi ya familia ni kisababishi kikubwa cha wasichana kukatisha masomo. Karibu asilimia 31% ya maoni ya wadau wa elimu hasa wazazi na wanafunzi wenyewe walidai umaskini kuwa ni sababu kubwa (HakiELimu 2010)[9]. Hali ngumu ya kiuchumi katika familia inasababisha yafuatayo:

4.1.2 Wazazi wanashindwa kuwatimizia watoto wa kike mahitaji yao ya msingi ya kimasomo. Hivyo, watoto wa kike wanakua wahitaji (shida) muda wote, na hivyo kuathirika kisaikolojia. Baadhi wanaamua kuacha shule na kubaki nyumbani ama kuolewa ili angalau wapambane na maisha wakiwa nje ya mfumo wa shule.

4.1.3 Wazazi kwenye kaya masikini wanawatumia watoto wa kike kama chanzo cha mapato kama vile ng'ombe na fedha. Lakini pia wanawatumia kufanya biashara ndogo ndogo ili angalau waingize kipato cha familia. Maana bila hivyo familia inakuwa katika hali mbaya kiuchumi hasa kukosekana kwa

[9] Wazazi walimu na wanafunzi waliohojiwa na wafanyakazi wa HakiElimu mkoa wa Tanga na Mara mwezi mei 2010 walibainisha ugumu wa maisha kuwa ni sababu kuu ya wasichana kukatisha masomo

mahitaji ya msingi kama vile chakula, na mahitaji mengine ya kila siku ya kifamilia. Wazazi wanatumia watoto wa kike kwa muda mwingi kufanya biashara maeneo mbalimbali[10]. Hivyo, watoto wa kike wanakosa muda wa kwenda shule. Na kwa sababu sheria ya elimu ya mwaka 1978 inatoa mamlaka kuwa mtoto asipohudhuria masomo kwa siku 60 mfululizo anapaswa kufukuzwa shule, watoto wengi wa kike wamefukuzwa shule na kukatishwa masomo yao kutokana na sababu hizo za utoro wakiwa wanafanya biashara za kuziingizia familia zao kipato[11]. Na wazazi wanadai kwamba wanawatumia zaidi watoto wa kike kwenye shughuli za biashara kwa sababu wao ni waaminifu zaidi kuliko wavulana kurejesha mapato kamili[12].

4.1.4 Umaskini wa familia umechangia sana watoto wa kike kujiingiza kwenye vitendo vya ngono ili kujipatia riziki toka kwa wanaume. Hali ngumu ya maisha ya familia kuwa chanzo cha wasichana kukatisha masomo ilielezwa pia na wasichana wenyewe, tuliofanya nao mahojiano mwezi Agosti 2011 katika Shule ya sekondari Forest Hill Morogoro, kama alivyonukuliwa mmoja wao..

> *"…..Tatizo hili linatokana na binti kukosa mahitaji muhimu na anapokuja shuleni anakuta wenzake wanavyo na anajikuta anapata vishawishi vya kufanya ngono na hatimaye kupata mimba. Pia kwa wengine ni tamaa, wanakuwa na tamaa ya vitu vizuri wanavyoviona wanataka wawenavyo wakati pesa hawana, hivyo wanajikuta wanajiingiza katika mambo ya ngono ili kupata pesa na vitu wanavyotamani kuwanavyo* (Mwanafunzi Kike Shule ya Sekondari Forest Hill, Morogoro).

**4.2 Uduni wa elimu inayotolewa na mazingira duni ya kujifunzia.** Ni sababu kubwa inayofanya wasichana wakatishe masomo yao. Shule binafsi zenye mazingira mazuri hata zikiwa kijijini watoto wengi hufanikiwa kumaliza shule na kunufaika nayo. Seminari na shule za dini ni ushahidi tosha. Ziko pembezoni mwa miji lakini watoto wanafanikiwa. Zile zenye mazingira duni na elimu duni inayotolewa huwakatisha tamaa watoto wetu hata zikiwa mijini watoto watakatisha masomo. Kama elimu inayotolewa hairidhishi, mtaala haushabihiani na mahitaji ya wanafunzi kimaisha au hauoneshi dalili za kuwanufaisha maishani wanafunzi hukata tamaa, na wazazi wanasita kusomesha watoto wao kwenye shule dhaifu.

**4.3 Malezi duni ya wazazi na tamaa za wasichana wenyewe.** Limetajwa na wazazi na wasichana wenyewe tuliofanya nao mahojiano mikoa mbalimbali ya Tanzania. Baadhi ya wazazi hawatumii muda mwingi kuwajenga watoto wao kimakuzi na kimaadili. Hivyo wasichana waliokosa maadili wanashindwa kujimudu *wana*iga na kufuata ushawishi mbaya. Makundi mabaya na makundi rika ambayo huwapotosha, wanajikuta mazungumzo yao ni vitendo vya ngono na mihemuko ya kubarehe inayowavutia kujaribu tendo la ngono linalowapelekea kupata mimba pasipo kutarajia. Nukuu hii ya mwanafunzi inathibitisha hili;

> ''..*Mimi ninavyoona ni tamaa za mwili, tunapofikia ule umri wa kupevuka tunakuwa na mihemko katika mwili ambayo usipojizuia utajikuta unapata ujauzito katika umri mdogo. Lakini yanazuilika kwa*

---

[10] Kama alivyosisitiza Mwalimu Lizy Ntipula wa Shule ya Msingi Mbuyuni Tanga kuwa, tatizo la wasichana kukatisha masomo mkoani humo linasababishwa zaidi na wazazi kuwatumia wasichana kwenye biashara.

[11] Mwalimu Mkuu Msaidizi wa Morembe Sekondari Musoma tuliyemtembelea mwezi Mei 2010 alifafanua kuwa hata shuleni kwake watoto wengi tu wa kike wameacha shule kwa sababu ya utoro, ambao kwa mujibu wa sheria ya elimu mwanafunzi asipohudhuria siku 60 anafukuzwa shule.

[12] Maoni yaliyosisitizwa na wazazi wa kata ya Mbuyuni Tanga mjini tuliofanya nao mahojiano sababu za wasichana kukatisha masomo mwezi Mei, 2010.

*kufanya kazi kwa bidii, kuwa bize na masomo na kufanya mazoezi* (Msichana, Shule ya Sekondari Forest Hill-Morogoro).

**4.3 Kukosekana kwa elimu ya afya ya uzazi.** Wasichana waliopevuka kimaumbile wanahitaji elimu ya uzazi ili wayapokee mabadiliko ya makuzi kwa umakini. Lakini inaonekana wazazi wengi hasa maeneo ya vijijini hawaongei na watoto wao wa kike ambao wako kwenye umri wa kukua. Bila wasichana kupewa maelekezo ya msingi kuhusu ukuaji wao na hasa namna ya kuepuka mimba wengi wamedumbukia kwenye mimba za utotoni bila kujua. Nchini Tanzania elimu ya afya ya uzazi haitolewi kikamilifu japo ni muhimu sana katika harakati za kuzuia mimba za utotoni. Kwa mujibu wa taarifa za uchunguzi wa idadi ya watu na afya, mimba za mapema zinahusiana moja kwa moja na ukosefu wa elimu na taarifa(TDHS 2004/05, Jedwali 4.9).

**4.3 Mitazamo kuwa thamani ya wasichana ni kuolewa/kuwa mama.** Ni chanzo kikubwa cha tatizo la mimba za utotoni. Bado kuna wanajamiii wana mtazamo kuwa mtoto wa kike thamani yake ni kuolewa ama kuzaa na kuwa mama. Wenye mitazamo hii ndiyo huwakatisha tamaa wasichana kusoma na kushiriki kwenye vitendo vya kuwavurugia maisha**.** Utafiti wa masuala ya Afya unaofanywa na serikali na wadau unabainisha ukweli huu ambao bado unaathiri jamii kubwa za kitanzania (TDHS 2004/05). Zipo sababu nyingi zaidi za tatizo hili, kama zilivyochambuliwa kwenye chapisho la HakiElimu la 2010 kuhusu "*Mbinu za Kuwasaidia Wasichana Kupata Elimu*".

**4.4** Mmomonyoko wa maadili ndani ya jamii na uduni wa sheria zetu ni chanzo kikubwa. Hili liko kuanzia kwa wazazi hadi walimu mashuleni wanaoshiriki kuwapa mimba wanafunzi. Fikiria, Mwalimu ndiye anayepewa dhamana ya kumlea mtoto, na anabeba majukumu yote; ulezi, kuwa mzazi pia kufundisha, hivyo ni BABA! Sasa baba kumpa mimba mtoto ni mwiko na fedheha kubwa katika fimilia ambayo ni shule na jamii[13]. Wapo pia wafanyakazi wa serikali na taasisi mbalimbali ambao wana dhamanya ya kuwaendeleza watoto wetu lakini nao wanachangia kuwapa mimba watoto wetu.

**4.5** Ni sisi wazazi na pamoja na serikali zetu ndiyo sababu kubwa za kushindwa kuthibiti tatizo hili. Maana sisi wananchi na serikali tumeiacha jamii ifanye inavyotaka juu ya watoto wetu wa kike na wa kiume. Wasichana wanabakwa na wavulana wanalawitiwa. Hakuna malezi wala ulinzi wowote toka kwa wananchi na serikali. Tofauti ni kwamba tu wavulana wao hawapati mimba, lakini wote tumewaaacha bila malezi ya kitaifa. Kupata mimba si kwa sababu wamevaa nguo fupi ama wana kiherehere[14], bali ni tamaa mbaya na ulafi mchafu wa baadhi ya wanaume husika wanaowapa mimba na kushindwa kuzishinda tamaa zao, ama kwa imani potofu. Ni wajibu wa taifa kukemea vitendo hivi, kutoa elimu ya kutosha kwa watoto na jamii kuhusu athari za mambo haya kwa taifa letu (Missokia, 2011).

## 5.0 Kwanini wanafukuzwa shule

Hadi sasa sababu kuu inayofanya watoto wetu wanaopata mimba wakiwa shuke kufukuzwa ni sheria ya elimu ya Mwaka 1978. Sheria hii inatekelezwa kwa kushirikisha kamati za shule, Afisa elimu wa mkoa na wilaya husika. Kamati za shule ambazo zinahusisha wazazi wa watoto wetu ndizo hufanya

[13] Maoni aliyosisitiza sana Mwanaharakati wa Elimu Elizabeth Missokia kuhusu maadili ya wazazi, walezi na walimu yanavyokuwa kikwazo cha maendeleo ya watoto wa kike kwa sasa

[14] Kuna Kiongozi mmoja wa ngazi za juu kabisa alisisikika akidai kuwa wasichana wanapata mimba kwa sababu ya kiherehere chao. Sio sahihi!

mikutano ya mwanzo kabisa kujadili hatma ya mtoto huyu hata kama hana makosa, kisha wanaamua kupeleka taarifa hizo kwa uongozi wa juu wa elimu. Kwa mujibu wa sheria ya elimu ya mwaka 1978 kifungu 35 na kanuni zake za mwaka 1978 na marekebisho ya 1995 na 2002 mtoto wa kike akipata mimba ni ushahidi tosha kuwa amefanya vitendo vya ngono vilivyo kinyume na sheria za shule hivyo anafukuzwa shule. Maelfu ya wasichana wa Tanzania wamekatisha masomo yao na kuharibu maisha kutokana na mimba za utotoni wanazopata bila hata ya kutarajia.




Wazazi walimu na hata Maafisa elimu wanaoshiriki kuwafukuza watoto shule kwa sababu ya mimba; wao wenyewe wana maoni tofauti kuhusu hatua hiyo. Jamii pana iko kwenye mjadala kwanini wafukuzwe shule watoto wetu? Lakini wengine wanahoji kwa nini wasifukuzwe shule wasichana wenye mimba? Mchanganuo wa maoni ya wengi kuhusu kuunga mkono kufukuzwa shule au kutounga mkono yako kwenye mitazamo binafsi ya mtu mmoja mmoja wala sio tafiti na ushahidi wa hali halisi. Baadhi ya mitazamo na maoni ya wananchi wanaotaka wasichana wanaopata mimba wafukuzwa shule na wale wanaokataa kitendo cha kuwafukuza shule yako kwenye maeneo haya: (Tazama jedwali chini)

***Jedwali: 1 Sababu za wanaotaka wasichana warudi shule baada ya kujifungua/na wale wasiokubali***

| Hoja za wanaounga mkono wasichana warudi shule baada ya kujifungua | Hoja za wanaokataa wasirudi shule/wafukuzwe moja kwa moja |
|---|---|
| • Itapunguza wajinga ndani ya jamii<br>• Itaongeza wataalamu na wazalishaji | • Kupotea kwa nidhamu shuleni<br>• Itashusha ubora wa elimu |

| | |
|---|---|
| • Kila mtu ana haki ya kupata elimu<br>• Elimu itawawezesha wasichana kuwalea vyema watoto wao<br>• Itaondoa pengo la usawa wa kijinsia kwenye elimu<br>• Itawapa nafasi wanawake kuchangia maendeleo ya nchi yao kikamilifu<br>• Wakirudi shule itakuwa ni njia ya kuzuia wengine kutopata mimba<br>• Adhabu ya kuwafukuza shule haiwasaidii kukua kiimani na kimaadili<br>• Wasamehewe na wapewe nafasi ya pili kuendelea na shule<br>• Wengi ni watoto hawajui lolote na hawajapevuka kiakili<br>• Baadhi wamebakwa bila kutaka, hawana hatia<br>• Adhabu ni kubwa mno zaidi ya kosa<br>• Hatujawaji kupata faida zozote kwa kuwafukuza wasichana<br>• Wengi wamerudi kwa kificho na wamefanikiwa sana | • Wasichana wata wadharau walimu wao, na kujiona wako sawa nao<br>• Itahimiza vitendo viovu vya ngono mashuleni<br>• Kutaongezeka magonjwa ya zinaa na UKIMWI<br>• Wasichana wenyewe hawatathamini elimu<br>• Wazazi watabebeshwa mzigo kulea wajukuu<br>• Ngono kabla ya kuolewa ni mwiko kwa mila zetu isiungwe mkono<br>• Ngono kabla ya ndoa ni kinyume na mafundisho ya dini<br>• Ni mzigo kwa serikali na wazazi usio na maana<br>• Ni tamaa zao, walitaka wenyewe<br>• Watapata mimba nyingine tena na itakuwa kupoteza fedha za bure |

*Chanzo: uchambuzi wa mwandishi wa maoni ya wadau waliohojiwa*

Ukiangalia kwa kina uchambuzi wa maoni ya wadau mbalimbali wa elimu, utakuta kuwa manufaa ya kuwarudisha shule wasichana ni mengi kuliko hasara zitakazojitokeza. Kimsingi maoni mengi yametawaliwa na mitazamo na hisia za watu kuliko tafiti. Lakini maoni haya yakizingatiwa yanaweza kusaidia sana kuboresha mikakati ya kuwarejesha watoto wetu shule baada ya kujifungua.

## 6.0 Wakifukuzwa shule wanakwenda wapi na watoto wao?

Ni hoja ya msingi ambayo kama jamii inapaswa tujiulize na kukusanya ushahidi ni wapi wanakokwenda watoto wetu waliopata mimba baada ya kufukuzwa shule. Je, wanaishia wapi? Wanafanya nini? jamii inawatazama vipi? Jamii inafaidika vipi na wao baada ya kurudi wakiwa wamekatisha masomo na ndoto zao kufifia? Baadhi ya kazi na mahali wanakokwenda wasichana waliokatisha masomo ni hizi:

**6.1** Wachache huolewa na kuendeleza familia zao wakiwa na hali nafuu au ngumu ya kiuchumi huku wakijitahidi kupambana na maisha na kuwasaidia watoto wao kupata mahitaji muhimu ya chakula, malazi na mavazi na kuwasomesha watoto wao. Baadhi wanaolewa wanafanikiwa na wengine hata wakiolewa bado maisha yanakuwa magumu sana, wanadharauliwa na wengine kutelekezwa kabisa

**6.2** Wengi hujiingiza katika ukahaba maisha yanapokuwa magumu na madhara ya ukahaba ni magonjwa. Na kupata magonjwa ndio mwanzo wa kuumiza familia kwa kugharamia matibabu. Wanakuwa ni mzigo tu kwa familia, kwa sababu yeye ni tegemezi na anaongeza mtu mwingine zaidi ambaye ni tegemezi.

**6.3** Kujihusisha na madawa ya kulevya na vitendo viovu kushindwa kujiendeleza kimaisha. Na hivyo, kuendelea kuzaa watoto wengi zaidi wasioweza kuwatunza na mzigo wa kuwatunza watoto wanapelekewa wazazi wao; yaani baba na mama yake wanaanza kulea wajuu wengi. Kama nukuu inavyothibitisha:

> "..*Wengine wanajiingiza katika uchangudoa, mimi nimeshawaona wasichana watatu ambao tulikua tunasoma nao wakapata mimba, wote wamekuwa machangu ili kujipatia pesa ya kujikimu na aendelee kupendeza* (Mwanafunzi wa Kike, Shule ya Sekondari Forest Hill, Morogoro Agosti 2011).

**6.4** Kwa sababu ya msongo wa mawazo juu ya hali yake, kufedheshwa na wanafamilia na kukata tamaa baadhi hujinyonga na walio wengi hujaribu kutoa mimba hizo kabla hawajazaa ili waokoe maisha yao ya shule. Wanaofanikiwa kutoa ni wachache, wanaopata matatizo hufa au kupata ugumba wa kudumu. Mathalani, hivi karibuni kuna mwanafunzi mmoja alijaribu kutoa mimba ili aendelee ma masomo akafariki dunia, jamii na wazazi walihuzunika sana (Nipashe Novemba 1, 2011).

**6.5** Baadhi wanakuwa wanafanya biashara ndogondogo kama kuuza mbogamboga, nyanya, matunda n.k. Wanafanya hivi sio kupata maendeleo bali kuhakikisha mkono unafika kinywani, na watoto wao wanapata chakula na mavazi ili wasongeze siku za kuishi. Ni wachache sana wanaofanikiwa kibiashara hadi kufikia kuwa wafanyabiashara wakubwa.

# 7.0 Tumefaidikaje na wasichana kufukuzwa shule?

Hakuna ushahidi wa wazi ndani ya jamii unaoonesha kuwepo kwa faida za kuwafukuza shule wasichana waliopata mimba wakiwa shuleni. Wakuu wa shule na walimu ambao kwa muda mwingi wamekuwa wakiwafukuza shule wasichana wadogo wanaopata mimba wanakubali kwamba hawajawahi kunufaika na chochote kwa kufanya hivyo[15]. Badala yake wanakiri kuwa wamekuwa wakichangia kukiuka haki za wasichana –hasa haki ya kupata elimu. Cha kusikitisha, maamuzi yao ya kuwafukuza shule wasichana yanawasukumia kwenye umasikini wa kudumu watoto wanaozaliwa na wasichana hawa, na hivyo kuendeleza duara la umaskini kwenye familia zao na taifa kwa ujumla. Watoto *wote* wana haki ya kupata elimu kwa kiwango wanachotaka

# 8.0 Hasara za kuwafukuza shule

Hasara za kuwafukuza wasichana na kuwazuia wasiendelee na shule baada ya kujifungua ziko wazi ndani ya jamii zetu, maana waliokatisha masomo wakarudi kwenye familia zao tunaishi nao, ni ndugu zetu na ni watoto wetu. Tunawaona wanachofanya na walivyoathirika na uamuzi huo juu yao. Baadhi ya hasara za kuwafukuza wasichana shule ni hizi:

**8.1 Kuwa tegemezi**. Binti akikatisha masomo anakua tegemezi kwa wazazi na hasa. Kuna wakati mwingine yule aliyempa mimba anamkataa na kumtelekeza kwa wazazi ambao wengi wao wanakuwa hawana uwezo wa kumudu maisha ya familia kubwa.

---

[15] Baadhi ya walimu wakuu kutoka Tanga, Tabora, Musoma, Meatu, Nachingwea, Sikonge, Lindi na Singida niliopata kufanya nao mahojiano vipindi tofautitofauti walidai hawaoni faida za kuwafukuza wasichana wenye mimba shule. Ni kuwaharibia maisha yao tu huku tatizo bado linaendelea.

**8.4 Kuathirika kisaikolojia**: binti aliyepata mimba na kufukuzwa anaathirika kisaikolojia maana yeye bado ni mtoto alafu amepata mtoto mwenzake. Hivyo anakuwa katika wakati mgumu sana wa jinsi atakavyomtunza mtoto. Na pia maneno ya watu watakavyokuwa wakimzungumzia mtaani atajihisi vibaya. Huathirika kisaikolojia kwa kusemwa semwa na watu na kuwachukia wanaume kwa kusababisha mimba na kuwatelekeza.

**8.5 Kushindwa kufahamu na kufuata kanuni za afya ya uzazi.** Wasichana wengi wanaokatisha masomo wanakosa fursa za kupata taarifa nyingi za kuhusu afya za uzazi na malezi bora ya watoto. Ndio maana wengi wao huzaa watoto wengi zaidi na zaidi huku wakiwa na changamoto nyingi za kiafya na kimaisha. Tofauti na wale walioelimika kikamilifu huwa na taarifa nyingi za masuala ya afya, na pia huweza kuzaa kwa utaratibu na mpango mzuri. Na wengi huzaa watoto wachache wanao wamudu na kutunza afya zao na watoto wao kikamilifu[16].




**8.6 Baadhi hujiingiza kwenye ukahaba na madawa ya kulevya**. Athari nyingine kwa mtoto wa kike anapokatisha masomo ni kujiingiza katika ukahaba maisha yanapokuwa magumu na madhara ya ukahaba ni magonjwa, na kupata magonjwa ndiyo mwanzo wa kuumiza familia kugharamia matibabu. Pia baadhi hujihusisha na madawa ya kulevya na kushindwa kujiendeleza kimaisha.

**8.6 Kifo wakiwa wadogo**. Baadhi hujiua au kufa kutokana na kufedheheshwa na wazazi, kujaribu kutoa mimba au wakati wa kujifungua. Wakifukuzwa wengi wanaishia kubeba mimba tena na kutoa,

[16] Utafiti wa Wizara ya Afya 2010 ulibainisha ukweli huu

kila akibeba mimba anatoa na wengine katika kutoa mimba wanapoteza maisha. Na baadhi huamua kujinyonga tu ili kuondoa aibu.

**8.7 Kurudisha nyuma maendeleo ya familia**. Wasichana wakikatiza masomo wanarudisha nyuma maendeleo yao binafsi, ya familia zilizowasomesha na jamii nzima au taifa kwa ujumla. Kumsomesha mtoto tangu shule ya awali hadi sekondari kuna gharama nyingi za moja kwa moja au za ziada. Wazazi hujidhiki kwenye masuala fulani ili kipato chao kigharamie elimu ya mtoto wao. Akifukuzwa shule pesa inapotea bure na yeye anageuka kuwa mzigo kwenye familia badala ya kuwa msaada kwenye familia.

**8.9 Wanakosa utaalamu, maarifa na kupoteza malengo**. Msichana anapokatiza masomo anakosa maarifa na utalaamu aliotarajia, na malengo yake yanakuwa yamevurugika kwa kiwango kikubwa. Na hivyo, kwa jamii ni anakuwa amepoteza fursa za kuongoza katika jamii maana hana elimu. Hili lilithibitishwa na wanafunzi wengi tulioongea nao, kama tunavyowanukuu baadhi yao mwezi Agosti mwaka huu:

> "…*ukiacha shule unapoteza malengo, tunaposoma tunakuwa na malengo ya kufika chuo kikuu na kupata kiwango fulani cha elimu, sasa unapoishia kidato cha pili au tatu unakuwa hujafikia lengo. Pia wazazi watakuchukia au kukunyanyapaa kwa sababu wametumia pesa zao nyingi kukusomesha alafu hujafanya lolote la maana* (Mwanafunzi wa Kiume Kidato cha Tano, Shule ya Sekondari Forest Hill, Morogoro, 2011).

> *"….Mimi naona kuwa atapoteza malengo yake ya baadaye kwa sababu tunaposoma tunakuwa na malengo ambayo tumekusudia kufikia, hata wazazi wanategemea hapo baadaye ukimaliza masomo na kuwa na maisha yako utawasaidia, hivyo binti kwa kukatiza masomo anakuwa kashindwa kutimiza lengo* (Mwanafunzi Kidato cha Nne, Shule ya Sekondari Forest Hill, Morogoro).

**8.10 Wanakuwa na maisha magumu kwa kukosa ajira**. Wakikatisha masomo wengi wanakosa ajira za kuwapatia kipato, na kwa taifa; ni kupoteza rasilimali watu ambao wangeweza kutumia elimu zao kwa manufaa yao na taifa kwa ujumla. Wazazi wenye watoto shuleni walibainisha mifano halisi kwenye jamii kama tunavyonukuu:

*"….Mimi nimeshawaona wengi tu, na athari zake ni kuwa na maisha magumu baada ya kujifungua inakuwa vigumu hata kulea mtoto inakuwa vigumu sana. Unakuta wengine wanajiingiza katika kazi ngumu zenye madhara kwa afya zao, kama kuuza pombe za kienyeji na ukahaba, na kujikuta anapata mimba tena na tena na kuwa na watoto wengi ambao hawezi kuwatunza na hii inawaharibia wale watoto maisha yao ya baadaye* (Mzazi wa Kike Morogoro).

*"…Mimi naona madhara yake ni kukosa kazi na kuishia kujiuza na matokeo yake asipokuwa mwangalifu anapata magonjwa ya zinaa. Kwa wazazi pia inawapelekea kupata aibu kuwa mtoto wao kaacha shule na anajiuza, na kwa sehemu anayotoka analeta watoto wa mtaani ambao hawahitajiki sana katika jamii kwa sababu wanachangia kuongeza umasikini katika taifa* (Mzazi wa Kike, TUPAWAKI, Morogoro).

## 9.0 Kuwarejesha shule baada ya kujifungua: tunaongozwa na ushahidi au mitazamo?

Unapofika mjadala wa kuwarejesha shuleni watoto wetu waliopata mimba kuna hoja nyingi zinazopingana na kukinzana. Hoja kubwa zimejikita katika makundi mawili. Kuna wale wanaodai wasirudi shule maana watakwenda kuharibu watoto wengine. Na wengine wanadai kuwa ni muhimu warudi ili wanufaike maishani na hawawezi kuwaharibu wengine.

Pamoja na wingi wa maoni ya wananchi juu ya kuwaresha darasani watoto waliozaa, hitilafu kubwa inayoonekana ni kwamba mjadala wa wanajamii wengi umetawaliwa na hisia, mitazamo, imani, na kasumba binafsi na sio tafiti[17]. Ukimuuliza anayesema kuwa kuwarudisha wasichana waliojifungua shuleni ni kuwaharibu wasichana wengine ni utafiti gani umethibitisha hilo? Ukiuliza kwamba watoto wa kike wanaweza kusoma na kufanikiwa wakipata tena nafasi, ushahidi gani umethibitisha hilo? Je, waliorudi shule walifanikiwa waliwaharibu wasichana waliowakuta? Haya maswali yote yanaweza kujibiwa kuwa kufanya utafiti kubaini ukweli na uhalisia wa jambo lenyewe, ili wote tuwe na mtazamo wa kujenga na wala sio kubomoa.




[17] Wachangiaji kwenye maoni ya wadau yaliyokusanywa na asasi ya Kuleana

## 10.0 Kwanini ni muhimu warudi shule / faida za kuwarejesha shule baada ya kujifungua

Yako manufaa ya wazi kabisa ya kusomesha watoto wetu hasawa watoto wa kike. Chapisho la HakiElimu lililochapishwa mwaka 2010[18] lilibainisha kinagaubaga faida hizo kwa wingi kutokana na maoni ya wanajamii waliohojiwa. Kimsingi faida za kusomesha watoto wa kike ziko kwa msichana mwenyewe, familia yake, serikali na jamii kwa ujumla. Baadhi ya faida za kurejesha wasicha shule baada ya kujifungua ni hizi:

**10.1** Wanaopata mimba wakiwa shule ndio kundi kubwa la nguvu kazi ya taifa wanaohitajika sana kuiendeleza nchi yetu. Kwa mujibu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu nchini Tanzania Vijana kati ya miaka 10 na 24 ni zaidi ya theluthi ya watu wote Tanzania, na wale walio chini ya miaka 30 ni asilimia 75 ya wananchi wote wa Tanzania (NBS 2009). Hivyo, vijana na watoto ndio nguzo ya taifa letu. Tusipowaelimisha wataindelezaje nchi yao? Wakiendelea kufukuzwa shule tutaendeleza kudhoofisha nguvu kazi ya taifa letu wenyewe na kushindwa kusonga mbele.




**10.2** Wakiendelea na masomo watajitambua zaidi maana wengi wanapata mimba wakiwa hawajitambui, watajua wafanye nini katika maisha yao hata kama wanafanya ujasiriamali wakiwa na elimu watafanya kwa makini.

---

[18] Chapisho hilo lina jina la "Mbinu za Kufanikisha Elimu kwa Wasichana" lilitolewa baada ya kukusanya maoni toka kwa wadau mbalimbali wa elimu kuhusu namna ya kuwasaidia wasichana wasikatishe masomo yao.

*"..Akipata elimu anapanua mawazo yake na anatambua fani yake, na atajikita kwenye fani yake kwa kujiajiri au kuajiriwa akishapata kazi ni faida kwa wazazi na hata kwa jamii nzima. Akisoma atapata kazi na anaweza kunitunza kwa sababu wazazi wengine tunakuwa na hali ngumu na elimu yake inamuwezesha kujitegemea yeye mwenyewe* (Mzazi wa kike, Morogoro Agosti 2011).

**10.3** Wakirejea shule na kuelimika wanakuza uwezo wa kufikiri na kujiamini. Kujiamini huko kunaendana na uwezo wa mtu kujua haki zake na wajibu wake katika jamii. Kujiamini katika kutoa maamuzi na kushiriki katika masuala yote ya kiuchumi kisiasa na kijamii. Ataweza kujiamulia mambo yake mwenyewe na kujitawala.

**10.4** Wakirudi shuleni watapata uwezo wa kutumia fursa zilizopo na kutengeneza fursa ili kujiletea maendeleo**.** Mfano ni fursa ya kuajiriwa na kujiajiri mwenyewe kutokana na maarifa na ujuzi alioupata. Maarifa ndiyo humuongoza mtu kutumia fursa zilizopo kama vile ardhi, madini, misitu, kubuni biashara, n.k. Bila elimu wanawake hawawezi kupata fursa nyingi wala kuzitumia fursa zilizopo kujiletea maendeleo yao na ya jamii.

"…*Ukimuelimisha mtoto mmoja wa kike ni sawa na umeelimisha watoto kumi na moja kwa sababu mtoto wa kike anafaida kubwa kuliko mtoto wa kiume, maana ana upendo na huruma sana kwa wazazi wake kwa hali na mali. Kwa mfano, kuna mama mmoja jirani yangu amesoma na ana watoto watatu ambao alifanikiwa kuwasomesha vizuri na sasa wanavyomuenzi huyo mama utapenda yaani wanamtunza sana mama yao hasa wale watoto wawili wakike ni raha tupu hadi mimi mwenyewe namtamani maana wa kwangu nilimuozesha na mahari nikala nikasahau kumbe ni bora ningemsomesha labda na mimi ningefaidika* (Mzazi wa kike, Morogoro Agosti 2011).

**10.5.** Wakirudi shule watakuza stadi za mawasiliano na kujiamini ili wawasiliane kwa usahihi na kwa manufaa. Stadi za mawasiliano ndizo msingi wa upashanaji habari. Msichana aliyesoma anakuwa na ujasiri wa kutoa maoni, kujieleza, kudadisi na kuhoji katika masuala yote yanayowahusu. Akifukuzwa shule anapoteza stadi hizi muhimu.

**10.6** Wakirudi shuleni watakuwa na nguvu ya kutambua na kuainisha mbinu za kupambana na changamoto zinazomkabili zikiwemo umaskini na maradhi, ambayo kwa kiwango kikubwa yanatokana na mifumo kandamizi inayobinya haki za wanawake.

**10.7** Wakiendelea na masomo baada ya kujifungua watapanua upeo wa ubunifu ambao unamsaidia kukabiliana na changamoto zinazowazunguka. Kuwawezesha kielimu wanawake kutawajengea nguvu hii muhimu ambayo wao na familia zao wataweza kujikwamua kutoka kwenye lindi la umaskini. Maana yanayojengwa ndani ya mtu ni maarifa tambuzi, maarifa matumizi na maarifa upanuzi[19]. Tunapowanyima elimu wasichana tunawanyima maarifa haya ambayo ni muhimu kwao ili waweze kuishi maisha ya neema.

*"….Faida tutakazo zipata ni kwamba akienda shule na kupata elimu anaweza kuwa msaada kwa taifa, kwa maana ya atakuwa mtaalamu kama vile daktari au akawa kiongozi bora katika taifa, pia atakuwa chachu kwa wadogo zake na ndugu wengine, akifanikiwa kwa kusoma, watu wataiga na kutamani kuwa kama yeye na hivyo kuleta mwamko kielimu na kimaisha kwa ujumla. Na kwa jamii na taifa anaweza*

---

[19] Aina za maarifa yanayojengeka kwa mtu, kama alivyofafanua mwanazuoni Peter Senge kwenye kitabu chake "Schools that Learn" cha mwaka 2000, uk 80.

*kuwa msaada kwa kutatua matatizo ya kijamii, kwa kutumia taaluma* yake (Mzazi wa Kiume, Lindi, 2011).

**10.8** Wakitendewa haki kwa kurejeshwa shuleni baada ya kujifungua watakuwa na moyo wa uzalendo kwa taifa lao na hisia za utaifa ambazo ni muhimu sana kwa jamii yeyote kupata maendeleo**.** Uzalendo ndio unaomchagiza mtu kufanya kazi bila kukoma ili kuiendeleza nchi, ndio unaoongoza haki na matendo halali katika ugawaji rasilimali na utoaji huduma. Uzalendo ndio unaojaza utaifa na kuithamini nchi yako badala ya nchi nyingine.

**10.9** Wakirudi shule baada ya kujifungua watapata fursa zaidi za kazi za kujiajiri na kuajiriwa, watajenga moyo wa kutambua umuhimu wa kazi, hisia za ari ya kufanyakazi kwa bidii na utashi wa kuthamini kazi. Maana kazi ndiyo msingi wa maisha[20]**.** Kuwafukuza shule ni kuwarudisha nyuma wanawake katika eneo hili kunawafanya washindwe hata kupata fursa za kazi, na hata wakipata zinakuwa kazi za kipato duni. Ni dhahiri hawawezi kuzifanya kazi kwa tija kubwa kama hawana elimu ya kutosha.

**10.10** Wakiendelea na masomo yao inawajengea uwezo wa kufanya maamuzi sahihi yenye mantiki na tija**.** Uwezo wa kufanya maamuzi yenye tija na yaliyo makini ni muhimu sana katika kufanikisha maisha kwa mtu yeyote. Kama wasichana/wanawake watashindwa kufanya maamuzi yenye tija ni hasara kubwa kwa jamii husika. Kwa mfano; wasichana wengi wasio na elimu wanashindwa hata kufanya maamuzi mazuri kuhusu miili yao na hadhi yao. Wengi wanatumiwa kama vyombo vya starehe na wanaume wasio[21] na hekima.

**10.11** Wakielimika watapiga kura kwa umakini zaidi. Kila uchaguzi unapofika wanawake ndio wengi kwenye foleni za kupiga kura. Na, wengi wao hasa waishio vijijini wanapiga kura pasipo kutambua umuhimu wa kura. Kwa hiyo, wanakuwa wanatumika kama daraja au ngazi za mafisadi kupandia kwenye madaraka au kujipatia fedha haramu. Elimu ndiyo suluhisho pekee la kuwafanya wanawake waweze kuwa na uwezo mpana wa kufanya maamuzi sahihi. Kuwafukuza shule ni kuongeza wapiga kura wasiojitambua.

**10.12** Wakirudi shule na kuhitimu masomo yao kutawajengea uwezo na uelewa mpana wa rasilimali za taifa na namna ya kuzitumia ili kujiletea maendeleo. Utambuzi na uelewa wa rasilimali za taifa ni muhimu sana kwa binadamu yeyote; maana bila kuelewa mtu hawezi kuzithamini rasilimali hizo, na wala hawezi kuzitumia ama kuzilinda[22].

**10.13** Kuwasomesha wasichana kutawafanya watambue misingi ya utamaduni wa taifa, mila na desturi za kitanzania pamoja na utamaduni wa mataifa mengine. Uelewa huu utawajengea wasichana utambuzi wa mila na desturi zetu nzuri, na kisha kuzilinda na kuziendeleza. Lakini pia kutambua utamaduni ni muhimu kwa sababu zipo mila na desturi zilizopitwa na wakati, ambazo zinafaa kuachwa. Kwa mfano, wanawake waliosoma na kupata elimu ni vigumu sana kwao kuendelea kukeketa watoto wao, au kuwaoza watoto wao wakiwa wadogo.

**10.14** Wakirudi shuleni hawatanyonywa wala kukandamizwa**.** Ni vigumu kwa wanawake waliosoma kunyanyaswa na wanaume katika jamii na taasisi zinazoendeleza mfumo dume na ukandamizaji wa

---

20 Hata kaulimbiu ya harakati za ukombozi wa Tanganyika ilikuwa ni “Uhuru na Kazi”

21 Hapa Tanzania wanaume kama hawa wanajulikana kama “Mafataki” lengo lao ni kuwaharibia maisha wasichana

22 Maoni ya wananchi wengi katika Kipindi cha cha HakiElimu cha Tafakari Time kilichorushwa na TBC mwezi Agosti na septemba kinabainisha ukweli huu

wanawake. Utamaduni ni utu wa mtu. Hivyo, elimu ni lazima iwajengee watu uelewa mpana wa utamaduni. Na hiki ni kigezo cha utaifa na umoja wa jamii yetu ya kitanzania. Bila kujua nyanja za utamaduni, mila na desturi zetu, ni rahisi sana kuburuzwa na tamaduni za kigeni, au kukandamizwa na desturi zisizofaa. Na hii inafanya watu wawe watumwa ndani ya nchi yao[23].

**10.15** Wakirudi shuleni kunawajengea uelewa mpana wa haki zao kama binadamu**.** Wanawake waliosoma watatambua haki zao zote kama binadamu na kama wanawake. Kujua haki zao ni ushindi mkubwa kwa mwanamke. Maana watakuwa na uwezo wa kuzilinda na kuzitetea kwa nguvu zote. Na wao hawatakuwa sehemu ya uvunjaji wa haki za watu wengine.
Ni ukweli uliowazi kwamba wanawake wengi wasiojua haki zao ndio wanaoendelea kukandamizwa. Elimu itawajaza uelewa huu! Pia itawachagiza kutetea hata haki za wengine na kubaini sheria na sera zinazowakandamiza na zile zinazowatetea. Bila elimu wanawake hawawezi kutambua haki zao. Na hivyo, ni vigumu kupata maendeleo yao wenyewe na ya jamii inayowazunguka. (UNDP: 2008, 2).

**10.16** Wakirudi shuleni na kuelimika watachangia ongezeko kubwa la pato la taifa na uzalishaji katika kilimo hasa kwa jamii zinazotegemea kilimo kama Tanzania. Tafiti zinaonesha mwanamke aliyesoma na kupata elimu uzalishaji wake katika mazao ya kilimo unaongezeka na kupunguza utapiamlo katika familia kwa asilimia 43. (Lisa & Haddad, 1995).

**10.17** Wakirudi shuleni na kupata elimu watajenga familia ndogo zenye afya, elimu na zenye ustawi bora wa utoshelevu wa mahitaji. Tafiti zinaonesha kwamba mwanamke aliyesoma ana uwezekano mdogo sana wa kuzaa watoto wengi ambao hawezi kuwapatia mahitaji yao ya msingi. Kwa mujibu wa utafiti wa bwana Raney, mwanamke aliyesoma ana wastani wa kuzaa watoto 2 hadi 3, ambao anaweza kuwahudumia kikamilifu. Lakini, mwanamke asiyesoma ana wastani wa kuzaa watoto 6-7 ambao wengi wao hasa katika mataifa masikini wanashindwa kuwahudumia vyema. (Subbarao & Raney 1995).

**10.18** Wakirudi shuleni kutachangia kwa asilimia kubwa kuokoa uhai wa watoto wengi, kupunguza utapiamlo na kupunguza vifo vya akina mama na watoto kwa asilimia 5-10. Maana msichana aliyesoma atakuwa mama wa watoto anayejua kanuni za afya, lishe ya mtoto na uzazi bora hivyo atailinda afya ya familia yake kwa umakini zaidi. Pia utafiti unaonesha kwamba ukiongeza uandikishaji wa wasichana shuleni kwa asilimia 10 tu unakuwa umepunguza vifo vya watoto 4 kati ya 1000[24]. Kama mzazi huyu alivyofafanua:

> *"….Afya ya mama na mtoto waliosoma inatofauti sana na ambaye hajasoma kiasi kwamba huwezi kulinganisha. Mwanamke aliyesoma anahudhuria kliniki kama inavyotakiwa na kutimiza kanuni nyingi sana za uzazi salama, na hii inatokana na elimu aliyonayo lakini pia kipato ambacho humuwezesha kumudu gharama za afya. Lakini yule ambaye hana elimu anakabiliwa na hali ngumu kifedha maana ile mia sita tu ya kumuona daktari anakwambia hana na anaamua kujitibu mwenyewe ananunua fansida anameza wakati hata hajapima malaria na matokeo yake anakuta haponi na hali inazidi kuwa mbaya anaanza kufikiri inawezekana ni taifodi na kuanza kuwaza kutumia muarobaini au alovera na madawa ya kienyeji badala ya kwenda hosipitali na matokeo yake wengi* wanakufa (Mzazi wa kike, Meatu, Machi 2011).

Wakiendelea na shule watajua namna ya kuwakinga watoto na maradhi, na kumfanya awe na afya muda wote. Atatumia vyema huduma za afya, ataboresha lishe ya mtoto, usafi wa mwili na mazingira

---

[23]Rais Kikwete mara nyingi amesisitiza kuwa Taifa lisilo na utamaduni wake ni taifa la utumwa.
[24]Ni sehemu ya Taarifa ya utafiti kwenye Kitabu kiitwacho "Women Education and Economic Well-being" Feminist Economics 1 (2): 21-46. Kilichoandikwa na Elizabeth King.

na atatumia uwezo na maarifa yake zaidi kujipatia kipato cha kuendeleza familia (Schultz 1993). Kwa faida kama hizi kwanini tusisomeshe watoto wa kike wote?

**10.19** Wakirudi shuleni baada ya kujifungua kunapunguza kusambaa kwa UKIMWI kwa kiwango kikubwa. Tafiti zinaonesha wanawake waliosoma wana asilimia kubwa ya kukwepa maambuzi ya UKIMWI na kuishi kwa muda mrefu. Maana wanapata taarifa zaidi kuhusu UKIMWI. Wanakuwa wanafahamu njia za kujikinga, wanakuwa na uwezo wa kujitambua na kufanya maamuzi kuhusu miili yao, na juu ya mahusiano yao na wanaume. "Wanawake wasiosoma wana asilimia kubwa zaidi ya hatari ya kuambukizwa UKIMWI kuliko wanawake waliopata elimu (Delamonica, 2000).

Hizi ni baadhi tu ya faida nyingi za kuwasomesha wasichana hadi wakafikia ndoto zao. Je tuendelee kukosa manufaa haya kwa watoto wetu wa kike kutokana kuwafukuza shuleni watoto wetu wanaopata mimba wakiwa wadogo bila kutarajia?

## 11.0 Wanarudi vipi shuleni baada ya kujifungua

Jambo la msingi linalopaswa kufanyiwa kazi na jamii kubwa ni kuamua na kupendekeza namna gani watoto wetu waliopata mimba na kujifungua wataweza kurudi shule. Kumekuwa na mkanganyiko wa maoni ya namna ya kurudi shule. Mapendekezo mengi yako kwenye maeneo yafuatayo:

1.1 Wapo wanaosema warudi shule zilezile walikuwa wakisoma baada ya kujifungua. Ushahidi unaonesha hakuna madhara kutekeleza hili japo kuna changamoto kadhaa: ikiwemo mazingira ya shule na mfumo wa mahusiano ya wanafunzi. Kuwarudisha wasichana waliozaa shule zilezile kutaondoa ubaguzi. Na tayari zipo nchi zilizofanikiwa kama Zambia[25] na Kenya ambako wengi wamerudi shule. Hata wazazi wengi tuliowahoji Mkoani Morogoro, Wilayani Kilindi Tanga na kwingineko walipendekeza warudi shule za kawaida. Nukuu ya mzazi huyu ni moja ya wanaounga mkono kurudi shule zilezile.




"…*Mimi nakubaliana warudi shule, lakini wasitengwe kwa sababu kwa kufanya hivyo utakuwa umewatenga na jamii ya wanafunzi wengine ambao wana haki ya kushirikiana nao katika masomo* (Mzazi wa Kiume, Tanga Mei 2010).

1.2 Baadhi wanapendekeza warudi shuleni, lakini wahamishwe na wawe kwenye shule maalumu ili wawe huru zaidi. Wanapendekeza hoja hii wana wasiwasi na kuchanganywa na wasichana wengine ambao hawajazaa bado. Japo hakuna ushahidi ulio wazi wa namna wasichana wadogo wanavyoweza kuathiriwa na mchanganyiko huo. Na ndani ya mfumo wa elimu jumuishi na utekelezaji wa Elimu kwa Wote mbinu hii inaweza kuendeleza ubaguzi kama haitatekelezwa vyema. Kama tulivyomnukuu Mzazi mmoja akipendekeza:

[25] Zambia wana sera maalum ya kuwarudisha wasichana shule baada ya kujifungua. Na hata Rwanda ina sera maalum kwa ajili ya elimu ya watoto wa kike inayoitwa "Girls Education Policy" ya mwaka 2008. Tanzania tunashindwa nini?

"…*Kwa hiyo kwa mimi kuliko kuwarudisha shuleni ni bora wawe na taasisi yao kama ile ya mama Clementina Foundation pale Moshi. Na mara nyingi watu kama hao wapelekwe bweni sio kutwa, hivyo serikali ishauriwe ijenge na kuboresha huduma za bweni hasa kwa wasichana ili kupunguza hali ya wao kuathirika na mazingira* (Mzazi, Musoma Mei 2010)


1.3 Baadhi wanapendekeza ziwepo shule maalumu za ufundi stadi za maisha ambazo watapelekwa wasichana waliojifungua kuendelea na masomo pia kupata ujuzi wa kimaisha. Shule hizi zitoe maarifa na ujuzi mbalimbali ili wamalizapo waweze kujiajiri na watakaoendelea na masomo wawe na uwezo wa kujiingizia kipato wakiwa bado wanasoma. Hii itaongoza mawazo ya kurejea kwenye tabia za mwanzo na kuwafanya wafanikiwe zaidi maishani.

## 12.0 Mbinu za kupunguza mimba kwa wasichana wadogo wa shuleni

Kuna mbinu nyingi zinazopendekezwa na wadau mbalimbali za kupunguza wasichana kupata mimba kama sio kulimaliza kabisa tatizo hili. Baadhi ya njia hizo tulielezea kwa kina kwenye chapisho letu la mwaka 2010 tulilolirejea mara kwa mara katika kitabu hiki. Baadhi ya maoni ya wataalamu na wananchi ni haya:

**12.1** Ni lazima sasa watoto wetu wasichana kwa wavulana wapewe elimu rika ya afya inayoendana na mabadiliko ya makuzi yao pamoja na uwezo wao wa kujitambua ili wawe tayati kuyakabili mabadiliko na kujikinga na mimba zisizo na utaratibu. Pia wanahitaji taarifa sahihi kuhusu afya ya uzazi na mahusiano ya kimapenzi miongoni mwao na huduma zinazoambatana na mahusiano hayo. Tafiti zinaonesha kuwa serikali ikiwekeza Sh Milioni 1600 tu kwenye uzazi wa mpango kunaweza kuzuia mimba za utotoni kwa wasichana wapatao 360,000 na kuokoa vifo vya akina mama 800 na kuokoa vifo 11,000 vya watoto wachanga (UNFPA 2004)[26]. Mbali na faida hizo kubwa kuwekeza kwenye elimu ya afya ya uzazi na uzazi wa mpango kunapunguza maambukizi ya virusi vya UKIMWi, hukuza usawa wa kijinsia, kunapunguza umaskini na kuongeza kasi ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

**12.2** Elimu itolewe kwa wazazi, wanajamii na kwa wanafunzi wenyewe kuhusu kujikinga na mimba za utotoni itasaidia kuondoa tatizo hili. Wazazi wajitahidi pia kuongea na kuwaelimisha binti [27]zao ili wajue hali ya maisha yao na waridhike na kile anachopewa na wazazi




[26] Hii ina maana kuwa iwapo serikali zetu zitatenga Sh milioni moja kila siku kwa miaka 5 kushughulikia uzazi wa mpango tu tunaweza kulimaliza kabisa tatizo la wasichana kukatisha masomo yao kwa sababu ya mimba zisizotarajiwa, maana idadi ya wasichana kukatisha masomo kwa sababu ya mimba haijawahi kufika hata 100,000 kwa mwaka.

[27] Wazazi ni shule ya kwanza ya mtoto, hivyo wakitekeleza jukumu lako kikamilifu watasaidia sana kukomesha mimba za utotoni

(Zombwe 2010). Pia wajue kwamba kama familia yao ni masikini wasome kwa bidii zaidi maana njia ya kuondoa umasikini ni elimu. Ugumu wa utekelezaji unatokana na uelewa mdogo kwa jamii, lakini elimu ikitolewa kwa wanajamii mambo yatabadilika, hivyo hata serikali ielekeze nguvu zake katika kuelimisha jamii sio tu kujadiliana bungeni na kuyaacha hukohuko huku wananchi wengi hawana elimu ya kutosha ya afya ya uzazi na manufaa ya elimu kwa wasichana.

**12.3** Kusaidia familia masikini kiuwezeshaji. Kama tulivyoona, wasichana wengi wanakatisha masomo kwa sababu za umaskini wa familia zao. Hivyo, lazima tutatue suala la umasikini wa familia, wazazi wawajibike zaidi katika kuwapatia watoto wao mahitaji muhimu. Serikali na mashirika waweke utaratibu wa kutoa ruzuku kwa wakulima vijijini ili wazalishe kwa faida. Pia kuwapunguzia ushuru wakulima na wafanyabiashara ndogo ndogo, hasa wanaouza mazao huko vijijini waondolewe ushuru wa mazao ili angalau wapate faida ya mazao yao iwasaidie kununua mahitaji ya familia. Pia kuwepo na ufadhiri wa moja kwa moja kwa wasichana wanaotoka familia masikini zaidi.

**12.4** Elimu ya stadi za maisha ifundishwe kikamilifu kwa wasichana na wavulana. Elimu hii huwawezesha wasichana na wavulana kuwa na utashi wa kufanya maamuzi yenye mantiki na tija kwenye nyanja zote za maisha yao kama vile wanataka kuwa akina nani baada ya kusoma, wanatamani utaalamu na kazi gani, wito wake ni nini, afya bora, lishe bora usalama wake na kuwajibika kijamii

**12.5** Kuboresha mifumo ya ufundishaji darasani na mbinu za kuwajengea stadi na ujuzi maisha, kuwajenga umoja na kupinga ubaguzi au kasumba za kudharauliana kutasaidia kukomesha mimba za utotoni. Tafiti zinaonesha shule zenye mifumo inayothamini michango ya wavulana wasichana kwa usawa, ujuzi wa ushawishi na kuthamini utu na ratiba zake za kujifunza, inakuza sauti za wasichana na wavulana kwa pamoja, na kukuza uwezo wa kufikiri kwa wote zina idadi ndogo sana ya wasichana wanaopata mimba au hakuna kabisa. Maana watakuwa wanajitambua na wataweza kujenga hoja na kujadiliana kwa kuelewa na kujitambua kwa kila hatua ya maamuzi yao na watajenga stadi za kutatua changamoto zilizombele yao kwa kufikiri kupita mipaka waliyoizoea.

**12.6** Kuweka mazingira rafiki ya kujifunzia hasa kwa wasichana ni jambo muhimu sana ili kupunguza au kuondoa mimba za utotoni. Ushahidi tunao; zipo shule nyingi binafsi hapa Tanzania ambazo wasichana hawapati mimba wala kukatisha masomo yao[28]. Na hili linaweza kufanyika kwa kuboresha miundombinu ya shule na kuifanya iwe rafiki. Mfano, kutenganisha vyoo vya wasichana na wavulana kwa umbali mkubwa, kuwepo na maji na vyumba vya usiri na kuwa na mbinu za ufundishaji pamoja na walimu ambao hawana mawazo ya kibaguzi au mawazo ya mfumodume, kuwepo na walimu na ufundishaji unaohimiza wasichana kujifunza na kuwatia moyo kufanikiwa sawasawa na wavulana, na pia kuwepo na walimu wanawake waliofanikiwa wawe kama mfano wa kuigwa kwa wasichana wadogo walioko shuleni hapo. Mbinu hizi zimeleta mafanikio makubwa sehemu zote walizotumia (UNESCO, 2010a).

**12.7** Kuwajengea uwezo watoto wetu wasichana kwa wavulana kufahamu stadi za kuthamini ujana na muda wao wa makuzi. Wasichana na wavulana wakifahamu thamani ya ujana na utoto wao wataweza kulinda thamani hiyo na hivyo mifumo ya shule inabidi ijenge stadi hizi kwa kuanzisha vikundi ambavyo ni muhimu sana kwa sasa. Kipindi cha kubarehe na kupata mabadiliko ya kimaumbile ni kipindi muhimu sana ambacho wazazi wanapaswa kutumia muda mwingi kuhakikisha watoto na vijana wetu wanapita kipindi hiki bila kuathirika, na wanufaike na makuzi yao. Kuzembea katika

[28] Mathalani shule nyingi zinazomilikiwa na kanisa Katoliki, ambako pia viongozi wengi hupeleka watoto wao hazina tatizo la wasicha kucha shule ama kupata mimba za utotoni. Kwa sababu malezi na mifumo ya shule hizo iko rafiki kwa wasichana na inawatia moyo kufanikiwa

kipindi hiki ndicho chanzo cha mimba zisizotarajiwa na kuharibika kwa watoto wetu –wasichana kwa wavulana.

**12.8** Kuelimisha kamati za shule na kuziboresha. Hili ni eneo muhimu sana kama tunataka watoto wetu wasikatishe masomo. Kamati za shule zinaundwa na wazazi wa watoto walio shule, lakini pia kamati za shule ndizo hukaa vikao vya mwanzo kabisa kujadili mtoto mwenye mimba afukuzwe. Chakushangaza, japo wazazi wengi wanaunga mkono wasichana wanaopata mimba waruhusiwe kurudi shule, bado wazazi hawa hawa wakiwa kwenye kamati za shule ndio wanaotoa mapendekezo ya kuwafukuza wasichana wenye mimba. Wakielimishwa watafanya kazi vizuri. Moja ya kazi yao ni kuhakikisha hata mtoto mmoja hakatishi masomo kutokana na mimba sio kuwafukuza watoto.

**12.9** Kuanzisha mabaraza ya wasichana wana harakati. Mabaraza haya yataongozwa na wasichana wenyewe mashuleni. Ndani ya kamati hizi za mabaraza ya vijana wasichana wao wataweza kukutana na wanawake waliofanikwa, wataweza kuhamasishana na kushauriana kuhusu masuala yanayowahusu, wataweza kukosoana kurekebishana kufuata njia bora zaidi za maisha, wataweza kujengeana uwezo na kuhakikisha sauti zao zinasikika kwa jamii pana. Wataweza kupendekeza maamuzi kwenye masuala yanayowahusu kwa umoja  wakanufaika wote. Na wataweza kutetea haki zao kwa umoja na upendo mkubwa. Sehemu walizofanya mabaraza haya kuna manufaa makubwa ambayo yameonekana wazi (FAWE, 2009).

**12.10** Utashi wa kisiasa ni muhimu sana kwenye suala la kuwarejesha watoto wetu shule na kuhakikisha mabinti zetu hawapati mimba za utotoni zisizotarajiwa. Wanasiasa licha ya tofauti zao za kiitikadi na kiajenda, bado wana mchango mkubwa katika hili. Maana ndio wanaotunga sheria, ndio wanaagiza maamuzi fulani yafanyike, ndio wanapitisha fedha za kwenye bajeti za serikali na ndio wanatunga sera ambazo aidha zinawaendeleza au kuwakandamiza watoto wetu, hasa wasichana. Utashi wa kisiasa kwa viongozi ni fikra zinazoona manufaa ya kutekeleza kwa vitendo sera, mipango, sheria na mikakati yenye kuleta manufaa kwa jamii pana. Nchini Tanzania, licha ya jamii kubwa kuunga mkono watoto wetu waendelee[29] na shule, bado utashi wa kisiasa ndio unasubiriwa kuamua hatma ya watoto wetu. Tunasubiri sera, sheria, mikakati na maagizo rasmi ya kuanzia kutekeleza sera ya watoto wetu kurejea shuleni baada ya kujifungua.

**12.11** Kuwekeza fedha kwenye elimu ya wasichana. Hii ni moja ya hatua kubwa ambayo itasaidia sana kupunguza ama kumaliza kabisa tatizo la wasichana kukatisha masomo. Tunahitaji kuwekeza kwenye elimu yao ya darasani, elimu ya makuzi, stadi za kimaisha na mazingira mazuri ya kujifunzia na kufundishia. Kuwekeza fedha za kutosha kuwaandaa walimu wenye ujuzi wa masuala ya jinsia na wasichana ili wafikapo shule wawasaidie watoto wetu wote kufanikiwa  kielimu na kimaisha[30]. Vifaa vya kufundishia na kujifunzia vilivyo rafiki kwa wasichana na wavulana ni muhimu viwepo shuleni. Na hili linaweza kufanywa na serikali, wazazi, wanaharakati na mashirika wahisani. Bila kuwekeza kwenye elimu ya watoto wetu kwa upana wake ni vigumu kulimaliza tatizo lenyewe.

**12.12** Tuandae na kuboresha mitaala yetu ili izingatie masuala ya jinsia na kuweka mazingira rafiki kwa wasichana na wavulana kuyachukulia kwa kina masuala ya jinsia ili wakue na ufahamu mkubwa

[29] Ziara ya kukusanya maoni mkoani Mara, Tanga na Morogoro iliyofanywa na wafanyakazi wa HakiElimu mwaka 2010 na 2011 ilidhihirisha kuwa wananchi wengi wanataka watoto wetu wanaopata mimba warudi shule baada ya kujifungua.

[30] Zipo shule za mfano hapa nchini ambazo zimewekeza kwa watoto wa kike na zimefanikiwa

kuhusu umuhimu wa kila jinsi kwa maendeleo ya jamii na kujenga umoja na amani ya nchi. Mitaala[31] iwajumuishe wanafunzi wote bila kujali tofauti zao. Mathalani, vitabu na silabasi, miongozo mbalimbali iandikwe kwa kuwagusa wasichana na wavulana, kazi za kujifunza shuleni zifanywe na jinsia zote, masomo yote yafundishwe kwa ukamilifu kwa wasichana na wavulana bila kuweka kasumba au mitazamo hasi kwamba baadhi ya masomo ni ya wasichana na mengine ni ya wavulana. Kuwa na mtaala unaowajumuisha wavulana na wasichana kwa mambo yote kutachangia kwa kiwango kikubwa kupunguza mimba za utotoni na kuwatia moyo wasichana kusoma kwa bidii na kunufaika na elimu inayotolewa shule (UNESCO, 2010 b).

**12.13** Turejeshe msingi wa maadili yetu kama jamii ya kuheshimu mahusiano ya tofauti za rika, ili kila mmoja atimize wajibu wake. Watoto wabaki watoto. Hili liendane na kuwepo kwa sheria kali ambazo zitafanya kazi. Sheria zichukue mkondo wake kwa wanahusika wanaowapa mimba watoto, wasionewe huruma hata kidogo[32]. Wasichana wafundishwe kujikinga, lakini inapotokea wa busara itumike kuwahoji watoto, waondoe woga na kuwataja wahusika ili wachukuliwe hatua na wazazi waelimishwe wasikubali hongo kuficha uhalifu huu. Ndipo tutalimaliza tatizo hili.

# 13.0 Wapo waliorudi darasani na wakafanikiwa

Licha ya sheria kukataza wasichana wenye mimba kurudi shule baada ya kujifungua, ni ukweli ulio wazi kwamba wapo wengi tu wamerudi shule kupitia mlango wa nyuma na wamefanikiwa kielimu na kimaisha. Maoni ya wadau na mifano mingi iliyotolewa na wananchi tuliofanya nao mahojiano yanathibitisha hili. Watoto wa wananchi na wale wa viongozi wamekuwa wakirudi shule wanapopata mimba, aidha kwa kuhamishwa shule au kupelekwa shule binafsi. Watu wenye uwezo wa kiuchumi na viongozi ndio wamekuwa mstari wa mbele kutekeleza suala la kuwarejesha shule watoto wao wanaopata mimba. Ila kinachofanyika sasa ni usiri, kificho na pengine kudanganyana sisi wenyewe kwa kufuata sheria kandamizi na inayowadidimiza zaidi wanyonge. Watoto wa masikini wasio na uwezo ndio wanaokosa fursa ya elimu pindi wanapofukuzwa shule, hawezi kwenda shule binafsi na wala hawawezi kutafutiwa fani nyingine ya kujiendeleza. Hivyo, madhara ya kuwafukuza wasichana wanaopata mimba ni makubwa zaidi kwa watoto wa masikini ambao wanahitaji elimu ili iwakomboe. Nukuu za baadhi wa wazazi tuliohojiana zina ujumbe kwa hili:


> *"..kwamba warudishwe shule baada ya kujifungua na niliona ilitokea kwa dada yangu ambaye binti yake alipata mimba akajifungua na akarudi kuendelea na masomo, alisoma vizuri hadi kidato cha sita akaeda chuo na akapata kazi nzuri na sasa ana maisha mazuri na anasomesha mtoto wake bila shida* (Mzazi wa kike, Liwale-Lindi 2011).

> *"..shida kubwa nionavyo baba ni ubinafsi na roho za uchoyo kwa baadhi ya viongozi wa serikali na watendaji. Wanajaribu kulifanya suala hili kama vile haliwezekani kumbe linawezekana. Mimi hadi nimefikia umri huu sijawahi kuona mtoto wakiongozi mkubwa amebaki nyumbani eti kwa sababu ya mimba. Wengi tu wanapata mimba na wazazi wao kwa sababu wana uwezo wanahamishwa shule na wanarejea kuendelea na masomo.*

31 Mtaala ni seti ya miongozo, maelekezo na mafunzo yanayotolewa kwa mfumo wa rasmi wa ujifunzaji. Kwa Tanzania mitaala inajumuisha miongozo, muhutasari, vitabu vya kiada, viongozi vya walimu, mada zinazofundishwa na mazingira ya ufundishaji

32 Missokia 2011

*Wanapenda kufukuza watoto wa wenzao lakini watoto wao wanarejea shuleni kila leo tunawaona* (Mzazi wa kiume, Tabora 2011)"




**Kisa mafunzo: yatima aliyebakwa na kufanikiwa kurudi shule baadaye**

Naitwa Dk. Maria nina umri wa miaka 38 ni Daktari bingwa wa Wanawake na watoto. Wazazi wangu wote wawili walifariki miaka 30 iliyopita. Niliachwa nikiwa mdogo na nikalelewa na mjomba wangu. Mke wa mjomba wangu alikuwa muuguzi kwenye Zahanati. Mjomba wangu na mke wake walikuwa watu wazuri na walinipenda. Sikuwa mtoto peke yangu niliyekuwa nalelewa hapo, alikuwepo pia mwipaye shangazi yangu yeye ni mvulana aliyekuwa na umri mkubwa zaidi yangu. Siku moja(miaka 23 iliyopita), nilitoka kuoga na nikaingia chumbani kwangu ili nivae nijiandae kulala, nilikuwa mimi na yule kijana mwipwaye shangazi yangu tu ndani ya nyumba. Mjomba na mke wake walikuwa safari. Yule kijana alikuja ghafla chumbani mwangu nikiwa bado napaka mafuta mwili wangu, kwa bahati mbaya sana chumba nilichokuwa nalala hakikuwa na kitasa kinachofunga, hivyo ilikuwa rahisi mtu kuingia na kutoka. Yule kijana alinilazimisha kufanya ngono sikukubali. Lakini kwa sababu alikuwa mkubwa na wenye nguvu zaidi yangu alinibaka. Nililia sana. Mjomba na mke wake waliporudi niliwajulisha kilichotokea. Yule kijana alitoroka nyumbani na hakuwahi kurudi tena hapo.

Nilikaa kwa miezi miwili nikiwa sina amani na mwili wangu. Na nilipoona sipati siku za hedhi nikahisi nina mimba. Mimba sio kitu unachoweza kukiweka pembeni na ukasahau, ni kitu unachoishi nacho kwa muda mrefu. Shangazi yangu baada ya kuona mabadiliko fulani kwenye mwili wangu, na kwa sababu yeye alikuwa ni muuguzi alinihoji maswali kadhaa na siku moja akaamua kunilaza kitandani na kunichunguza. Aligundua nina mimba ya miezi minne. Mjomba wangu alikasirika sana, hadi ikanifanya nione dunia hii haina maana tena kwangu. Mjomba aliniambia hatanisaidia tena kwa lolote kwa sababu nina mimba, na nikifukuzwa shule nitafute pa kwenda. Niliwakumbusha kuwa miezi michache iliyopita nilibakwa tena humu humu ndani nadhani ndiyo sababu ya mimba hii. Siku iliyofuata sikuwa na ujasiri wa kwenda shule, maana nilijua shule ndiyo mwisho.

Mke wa mjomba alikweda shule kuwaeleza kuwa nina mimba. Mkuu wa shule akaniita ofisini kwake nikiwa na shangazi yangu (mke wa mjomba). Mkuu wa shule alikuwa na busara sana. Akasikitika yaliyonipata na akashauri kuwa nina uwezo mkubwa shuleni. Hivyo, ni lazima nifukuzwe shule maana ndiyo sheria inasema hivyo. Lakini akanishauri nikisha zaa yeye mwenyewe ataongoza zoezi la kutafuta shule ili nirudi darasani baada ya kujifungua, shangazi yangu alifurahi pamoja nami. Nikarudi nyumbani nikajifungua mtoto wa kike, na baada ya miezi sita ya kujifungua nikarudi shule (tofauti na niliyosoma ila kwa kificho na nikarudia darasa. Nilisoma kwa bidii sana na nikawa mtu wa kwanza kila mtihani. Nikafaulu kidato cha nne na kwenda kidato cha tano tena masomo ya sayansi ambayo inasemekana wasichana wengi hawayapendi-nilisoma Fizikia, Chemia na Baiolojia (PCB). Nilifaulu pia na kwenda Chuo Kikuu cha Dar es salaam. Na sasa nina shahada mbili za Udaktari. Nimetibu maelfu ya watanzania wenzangu na bado naendelea kuwatibu. Watoto wangu wawili wako sekondari na yule mkubwa (niliyemzaa niko shule) anamaliza kidato cha sita mwaka ujao (2012) mdogo wake anasoma shule nzuri. Familia yangu haina shida na pia walezi wangu nawakumbuka na kuwasaidia pia. Nina furaha na Amani. Ninachoweza kushuhudia katika hili ni kwamba iwe kwa kujua au kutojua kuwafukuza wasichana wanaopata mimba bila kuwa na mikakati ya kuwarudisha shule ni kuiangamiza nchi. Mimi ni mfano huo, nisingerudi shule nisingeweza kuwatibu watanzania wenzangu maelfu kwa maelfu kama ilivyo sasa. Na wazazi wana mchango mkubwa sana katika hili (Dk Maria, Dar es salaam 2011).

------------------------------------------------------------------------------------------------------------

***Sehemu ya wasifu wa daktari Mary kutoka moja ya hospitali kubwa hapa nchini tuliyehojiana naye mwezi Septemba mwaka 2011 Jijini Dar es salaam**.*

## 14.0 Hitimisho na Mapendekezo

Hakuna njia ya mkato ya kumaliza tatizo la watoto wetu kupata mimba na kukatisha masomo bila kufikiri kwa kina, kuunganisha juhudi na kuamua kufanya maamuzi magumu ili kunusuru watoto wetu. Muda wa malumbano, mabishano na kulidharau tatizo na kujifanya halipo umekwisha. Maana tangu tuanze kulumbana na kulaumiana hakuna hatua ambazo zimeonekana zinaweza kupunguza tatizo hili kwa kiwango tarajiwa. Jitihada nyingi tumeziweka kwenye kuwalaumu[33] waathirika wa tatizo na mifumo yetu badala ya kutafuta suluhu za tatizo hili.

Ni muhimu pia ikumbukwe kwamba suluhu ya tatizo hili haiwezi kutoka hewani au kutoka nje ya watanzania wenyewe. Dawa ya tatizo hili tunayo sisi wenyewe watanzania. Na hatua ya kwanza ni kulitambua tatizo kwa kina na athari zake, kufanya tafiti na kukusanya taarifa sahihi kuhusu athari na ukweli wa mambo kuliko kufuata imani, mitazamo yetu na hisia zetu huku ukweli dhahiri ukiendelea kufichwa. Kama tunaamini wanawake nchini Tanzania ni wengi zaidi kwenye jamii zetu na wana mchango mkubwa sana kwenye maendeleo ya nchi yetu, hatuwezi kukwepa jukumu kubwa tulilonalo la kuhahakisha watoto wetu wa kike wanaopata mimba wakiwa shuleni wanarejea darasani na kuendelea na masomo baada ya kujifungua. Sio nadharia wala dhahnia! Sio ndoto wala ajuza. Ni kitu cha ukweli na kinawezekana. Nchi kadhaa ulimwenguni zimefanikiwa zikiwemo za majirani zetu Wakenya, Zambia na Rwanda, sisi tunaweza kutekeleza sera hii kwa uzuri zaidi maana tayari tuna

[33] Kama tulivyomsikia Mkuu wa Mkoa akidai wasichana nao wakamatwe wawekwe ndani ili wawataje waliowapa mimba. Gazeti la The Guardian Novemba 1, 2011

fursa nyingi kama vile shule nyingi na nyenzo za kutosha za kujifunzia pia tuna umoja na amani ndani ya nchi yetu.

Kuendelea kulipuuza tatizo na kubaki kuliongelea tu bila kuchukua hatua thabiti kivitendo ni kuirudisha nyuma nchi yetu kimaendeleo. Maana kama wananchi wengi hawatapata elimu kikamilifu nchi itakosa wataalamu, wazalishaji kwenye sekta muhimu za uchumi. Ni bora tukwepe gharama za kukabiliana na ujinga kwa kuwekeza kwenye elimu ya watoto kikamilifu ikiwa ni pamoja na kuwarudisha shule watoto wetu wanaopata mimba wakiwa wadogo shuleni. Hili linawezekana tukiungana na kuamua, walioweza ni binadamu kama sisi. Ni nia na utashi tu!

# Marejeo


Aidoo, A.A. (1981), "Ashante Queen Mothers in Government and Politics in the Nineteenth Century." In F.C Steady, ed., The Black Woman Cross-Culturally. Cambridge, MA: 65-77.

BEST Basic Education Statistics in Tanzania 2006-2010, National Data, Ministry of Education and Vocational Training

Bishop, G. (1986). *Innovation in Education*. London: Macmillan Educational

Deborah Tannen (1992) *How Schools Shortchange Girls*. The study of major Findings of girls Education. Marlow and Company. USA

Gilligan C (1982) *In a difference Voice*. Psychological Theory and Women Development. Harvad University Press

HakiElimu. (2007a). *Five years (2002-2006) of PEDP implementation: Key findings from official reviews.* Dar es Salaam: HakiElimu.

HakiElimu. (2007b). *Two years of SEDP implementation (2004-2006): Key findings from government reviews.* Dar es Salaam: HakiElimu.

Independent Evaluation Group. (2006a). *From schooling access to learning outcomes: An unfinished agenda. An evaluation of World Bank support to primary education.* Washington DC: World Bank Group.

IRIN Africa. Tanzania Demographic and Health Survey, 2005. UN Office for the Coordination of Humanitarian Affairs 2007.

Kuleana, (haujulikani mwaka) *Hodi Tena Darasani*. Wasichana waliopata mimba ruksa kurudi darasani? kituo cha kutetea haki za watoto, Mwanza

FAWE (1995) School Drop out and Adolescent pregnancy, Africa Education Ministers, Nairobi

Juddy Maan (1994) *The difference*. Growing up female in America; Time warm Company.USA

Hill, M.A. and King (1995), Women's Education in Development Countries: Benefits and Policies, Baltimore: Johns Hopkins.

Klasen, Stephan (1999), "Does Gender Inequality Reduce Growth and Development? Evidence from Cross-Country Regressions", Policy Research Report on Gender and Development Working Paper series, No. 7, Washington DC: World Bank.

Klasen, Stephan (2002), Low Schooling for Girls, Slower Growth for All? Cross-Country Evidence on the Effect of Gender Inequality in Education on Economic Development", The *World Bank Economic Review* 16(3), 345-373.

National Bureau of Statistics (2009) Tanzania in Figure, Dar es salaam

Nyerere, J. K. (1968). "Education for Self-Reliance", in *Freedom and Socialism, Uhuru na Ujamaa*, Oxford University Press, Oxford

Subbarao, K., and Laura Raney (1995), "Social Gains from Female Education." Economic Development and Cultural Change 44(1): 105-28.

TAMWA (2010). *Report on School Girls Pregnacy Survey* in 17 regions of Tanzania

TENMET (2011) A Review of Gender Based violence in schools in Tanzania. An education stakeholders report

TEN/MET (2007)Strengthening Education in Tanzania: CSO Contribution to the Education Sector Review 2007

Uchendu, Victor (1965), The Igbo of South-Eastern Nigeria. New York

URT (2003) Tanzania Development Vision 2025

UNESCO (2010a) Gender Responsive Budgeting in Education; UNESCO Asia and Pacific Regional Bureau of Education

UNESCO (2010a) Gender Issues in Higher in Education; UNESCO Asia and Pacific Regional Bureau of Education


URT (2000b) *National Policy on Community Development Gender*: Ministyr of Community Develpoment Gender and Children


UN, Tanzania (2010) Prevent adolescent pregnancies and keep girls in school!

Uwezo, TEN/MET & TWAWEZA (2011) are our children learning? Annual learning assessment report

Zombwe G (2009) *Women are the Catalyst of Development.* Empowering them is a quick path to socio-economic Development. HakiElimu, Dar es Salaam

Zombwe G (2010) *How can Parents help a Child to Learn*? Home is the Child's first School. HakiElimu, Dar es Salaam



HakiElimu inawawezesha wananchi kuleta mabadiliko kwenye elimu na demokrasia

S.L.P 79401 ● Dar es Salaam ● Tanzania
Simu. (255 22) 2151852/3 ● Faksi (255 22) 2152449
info@hakielimu.org ● www.hakielimu.org